Maswali Yanayoulizwa Sana ya One&All

Ujasiriamali Jumuishi wa Eneo la Lansing

Mpango huu mpya wa ujasiriamali ulianza vipi?

One&All ni mpango ulioundwa na kutolewa na Lansing Economic Area Partnership (LEAP Ushirikiano wa Kiuchumi wa Eneo la Lansing) na unafadhiliwa na Michigan Economic Development Corporation (MEDC Shirika la Maendeleo ya Kiuchumi ya Michigan) na Consumers Energy Foundation. LEAP ni shirika lisilo la kiserikali na lisilozalisha faida linalohudumi kukidhi mahitaji ya maendeleo ya kiuchumi ya kaunti za Clinton, Eaton na Ingham.

One&All ni nini?

One&All ni mpango jumuishi wa ujasiriamali kwa watu wanaotamani kuanzalisha na kukuza biashara, lakini hawana rasilimali muhimu za kifedha na mahusiano ya watu na biashara nyinginezo. Lengo la One&All ni kuongeza mtaji kwa kuwasaidia watu katika kaunti za Clinton, Eaton, Ingham na Shiawassee walio kwenye au chini ya kiwango cha Asset Limited, Income Constrained, Employed (ALICE Waajiriwa Waliopungukiwa na Rasilimali na Mapato), wanaojulikana kwa kawaida kama maskini wanaofanya kazi.

One&All inawapa washiriki mchanganyiko wa kipekee wa mafunzo na ukufunzi wa biashara katika mpango wa miezi 2, huku pia ikiwaunganisha washiriki na wataalam wa biashara na ufadhili wa kifedha.

Maombi yanapatikana kwa njia ya kielektroniki na fomu ya karatasi kwenye http://www.purelansing.com/oneandall. Mipango ya One&All hudumu kwa vipindi vya miezi 2. Waombaji wanaweza kuchagua kipindi kinachowafaa zaidi kulingana na ratiba zao wakati wanawasilisha ombi.

One&All hufanya kazi vipi?

Mpango wa One&All utaendelea kwa miaka 2 ukijumuisha vipindi kadhaa vya miezi 2 na mtaala wa vikao vya vitendo na vya kina kuhusu changamoto za biashara. Katika kipindi chote hiki, washiriki watapata mwongozo na usaidizi kutoka kwa wakufunzi waliojitolea kuwawezesha kufanikisha dhana ya biashara au mkakati wa ukuaji.

Waombaji watakuwa na nafasi ya kuchagua muhula wa mpango kulingana na ratiba yao wakati wa kuwasilisha ombi.

Tarehe za mpango huu ni:

- Agosti 2020 – Oktoba 2020
- Januari 2021 – Machi 2021
- Mei 2021 – Julai 2021
- Agosti 2021 – Oktoba 2021
- Januari 2022 – Machi 2022
- Mei 2022 – Julai 2022

Ni kiasi gani cha ufadhili kinachopatikana kwa kila mshiriki wa mpango huu?

Kila mshiriki ambaye anakamilisha mpango wa miezi 2 atapata ruzuku ya $2,500.

Fedha za ruzuku zinaweza kutumiwa kwa njia gani?

Fedha za ruzuku zinaweza kutumiwa kwa busara ya kila mshiriki ili kulipia gharama zinazohusiana na kuanzisha au kukuza biashara, ikijumuisha, lakini si tu: gharama za kisheria, utangazaji na mawasiliano, mahitaji ya vifaa na mahitaji mengine.

Je, ninapaswa kukamilisha kipindi cha miezi 2 ili nipate ruzuku?

Ndiyo, sharti ukamilishe kipindi cha miezi 2 ili upate ruzuku ya $2,500.

Je, ni sharti niwe mkazi wa eneo la Lansing ili nishiriki katika mpango wa One&All?

Ndiyo, sharti uwe mkazi na biashara yako sharti iwe katika eneo la Lansing (kaunti za Clinton, Eaton, Ingham, au Shiawassee) ili ushiriki katika mpango huu.

Mikutano ya mpango huu itafanyiwa wapi?

Vipindi vya mafunzo, mikutano na shughuli zingine zote zitafanywa katika mazingira salama katika jumuiya za wateja wetu. Mpango wa kwanza mwezi Agosti wote utafanywa mtandaoni. Timu ya One&All itakusaidia kufahamu kabisa mifumo yote ya mtandaoni inayotumika.

ALICE ni nini?

Kiwango cha Asset Limited, Income Constrained, Employed (ALICE Waajiriwa Waliopungukiwa na Rasilimali na Mapato) ni kiwango halisia kilichoundwa kutokana na Bajeti ya Kukimu Familia. Kiwango hiki kinakadiria gharama ndogo zaidi ya mahitaji matano msingi ya familia, ikijumuisha makazi, malezi ya watoto, chakula, usafiri na huduma ya afya.

Kiwango cha ALICE kinajumuisha familia zinazopata ufadhili unaozidi Kiwango cha Umaskini cha Kitaifa lakini chini ya gharama ya msingi ya maisha katika jimbo hili. Familia milioni 1.66 katika jimbo la Michigan (43% ya familia za Michigan) kwa sasa haziwezi kukidhi mahitaji yao ya msingi ya familia.

Mapato ya familia sharti yawe chini ya kiwango cha chini kinachotambuliwa cha kukidhi mahitaji ya msingi ya familia, ambacho ni zaidi ya $21,000 kwa mwaka ($10.52 kwa saa) kwa familia za mtu mmoja mzima na zaidi ya $61,000 ($30.64 kwa saa) kwa familia ya watu wanne.

Je, nitajuaje kama ninatimiza masharti ya One&All?

Unatimiza masharti ya One&All ikiwa uko katika kiwango au chini ya kiwango cha ALICE na jibu lako maswali haya ni ndiyo:

- Je, unapanga kuzindua biashara au kufanikisha biashara yako?
- Je, ungependa kupokea mafunzo na ukufunzi wa vitendo na halisia katika kikundi cha wajasiriamali wengine kama wewe?
- Je, uko tayari kukosolewa ili kufaidi biashara yako?

Timu yetu iko tayari kila wakati kuzungumza na wewe kuhusu biashara yako kabla uwasilishe ombi. Unaweza kuwasiliana na Jerry Norris wa Fledge kupitia jerry@thefledge.org au (517) 230-7679 AU Erika Brown wa Refugee Development Cente kupitia ebrown@rdclansing.org na 562-290-3660.

Je, ni dhana za aina gani ambazo One&All inatafuta?

One&All inatafuta dhana kutoka kwa tasnia zote - ikijumuisha mashirika yasiyo ya faida.

Je, ninahitaji mpango wa biashara?

Mpango wa biashara hauhitajiki. Unahitaji kutuonyesha shauku na bidii yako na kuthibitisha kuwa umefanya utafiti wa awamu za kwanza.

Je, mshirika wangu wa biashara au timu nzima inahitaji kushiriki?

Mwanzilishi mwenza mmoja anapaswa kuwa mwakilishi na kujitolea kuhudhuria vikao vyote, mikutano ya wakufunzi na hafla. Ni bora ikiwa waanzilishi wote watahudhuria mahojiano ya kwanza, ikiwezekana. Ni muhimu kwa biashara yako, lakini si lazima, kwa washirika wengine wa biashara kujiunga kwa mikutano mingine ya mpango.

Je, biashara yangu inayomilikiwa na kampuni kuu inakubaliwa?

Hapana, biashara yako sharti isiwe wakala au tawi la mfumo wa kitaifa.

Je, mashirika yasiyo ya faida yanakubaliwa?

Ndiyo, mashirika yasiyo ya faida ambayo yanakubaliwa ikiwa yanakidhi masharti ya kuwasilisha ombi.

Je, biashara zinazomilikiwa na mtu mmoja au biashara zinazoendeshewa nyumbani zinakubaliwa?

Ndiyo, biashara zinazomilikiwa na mtu mmoja na biashara zinazoendeshewa nyumbani zinakubaliwa ikiwa zinakidhi masharti ya kuwasilisha ombi.

Je, kutakuwa na kipindi maalum cha kuwasilisha ombi?

Tunatarajia kuwa maombi ya ruzuku ya mpango huu yataanza kupokewa Jumanne, tarehe 30 Juni. Maombi yatakubaliwa na kukaguliwa mfululizo hadi nafasi zote yajazwe. Itakuwa bora ikiwa utajaribu kuwasilisha ombi mapema ili uongeze nafasi yako ya kukubalika.

Ni watu wangapi watachaguliwa kwa kila kipindi cha mapngo hii?

Kati ya Agosti 2020 na Julai 2022, mipango sita ya miezi 2 itafanyika. Kila mpango utajumuisha watu wasiopungua 20.

Nitatumaje ombi langu?

Ombi litapatikana katika muundo wa mtandao na nakala ya chapisho kwenye purelansing.com/oneandall. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kujaza fomu ya ombi, wasiliana na Refugee Development Center (Kituo cha Ustawi kwa Wakimbizi) upate usaidizi wa lugha nyingi au The Fledge upate usaidizi wa kibiashara.

Nitawasiliana na nani ili nipate maelezo zaidi?

Ikiwa unahitaji usaidizi wa lugha nyingi wakati wa kujaza fomu ya ombi, tafadhali wasiliana na Refugee Development Center. Ikiwa una maswali mengine kuhusu mpango huu, tafadhali wasiliana na The Fledge.

Usaidizi wa Lugha
The Refugee Development Center (Kituo cha Ustawi kwa Wakimbizi)
refugeedevelopmentcenter.org

Erika Brown
(562) 290-3660
ebrown@rdclansing.org

Usaidizi wa Kibiashara
The Fledge
thefledge.com

Jerry Norris
(517) 230-7679
jerry@thefledge.com

Maswali ya Jumla kuhusu Mpango
Ushirikiano wa Eneo la Lansing (Ushirikiano wa Kiuchumi wa Eneo la Lansing)
purelansing.com/oneandall

Anum Mughal
anum@purelansing.com